JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

TAARIFA YA USHIRIKISHWAJI JAMII NA WADAU WA MABORESHO YA SOKO LA TEMEKE STIRIO

HADI

MACHI 2020

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke
S. L. P. 46343
Dar es Salaam.

YALIYOMO

YALIYOMO i

UTANGULIZI 1

USHIRIKISHAJI JAMII/WADAU 1

MAELEZO YA MRADI 1

HATUA YA 1: MADHUMUNI YA USHIRIKISHAJI JAMII/WADAU 4

HATUA YA 2: UTAMBUZI WA JAMII/WADAU 4

HATUA YA 3: UCHAMBUZI WADAU KWA KUZINGATIA KIPAUMBELE 4

HATUA YA 4: NJIA (MBINU) ZILIZOTUMIKA KUSHIRIKISHA JAMII NA WADAU 5

Mikutano ya jamii 5

Mahojiano ya Mtu mmoja mmoja 5

Majadiliano ya Vikundi (focus group discusion) 6

HATUA YA 5: UFUATILIAJI NA USHUGHULIKIAJI WA MALAMIKO/KERO ZA WADAU 6

HATUA YA 6: TAARIFA ZA MASWALA/MICHANGO/MAONI YALIYOIBULIWA NA WADAU KATIKA HATUA ZA USHIRIKISHWAJI JAMII 6

Jedwali na 2. 7

MAONI YA WAFANYABIASHARA WA SOKO LA STERIO 10

Hitimisho: 11

UTANGULIZI

Soko La Temeke Sterio ni miongoni mwa miradi ya uwekezaji kwa kushirikiana na Sekta binafsi kwa lugha ya kigeni **'Public Private Partnership (PPP)**. Benki ya Dunia kwa kushirikiana na wadau wengine wanasaidia hatua kwa hatua uwekezaji huo kupitia Kitengo cha Ofisi ya Rais **TAMISEMI** cha Uwekezaji kwa kushirikiana na Sekta binafsi inayoitwa **PPP – Node (PO RALG)**.

Aidha Ujenzi wa soko la sterio ni miongoni mwa miradi **22** inayotarajiwa kutekelezwa katika Halmashauri mbalimbali zinazohusika, Miradi hii yote ni ya kwanza **(22 Fist mover PPPs).** Hatua mbali mbali zimefanyika za maandalizi tangu mwaka juzi (Disemba, 2017) mpaka sasa.

Oktoba 2018, upembuzi yakinifu wa awali umekamilika na vikao vya Halmalshauri tayari vimebariki na kupeleka barua kwa Katibu Mkuu TAMISEMI ili kuipitia na kutoa maoni na maelekezo kwa hatua inayofuata. Baada ya hapo, utafanyika upembuzi yakinifu wa kina chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

USHIRIKISHAJI JAMII/WADAU

Taarifa ya Ushirikishaji Jamii na Wadau ni muhtasari wa shughuli mbalimbali zilizotekelezwa ili kupata maoni/mapendekezo kuhusiana na Uboreshaji wa Soko la Temeke Stirio katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Shughuli hizi zilitekelezwa kati ya 2017 hadi Disemba 2019.

Ili kufanikisha ujenzi wa soko jipya, itahitaji kuwaondoa kwa muda wafanyabiashara wa sasa katika soko na kuwahamishia katika eneo ambalo wataendeleza shughuli zao za biashara wakati wa kipindi chote cha ujenzi. Zoezi la ushirikishaji jamii/wadau umelenga katika kufanya mazungumzo na kupata maoni ya wafanyabiashara hawa katika soko la Temeke Stirio, pamoja na wadau wengineo kama vile majirani, watumishi na viongozi walio jirani na eneo ya mradi.

Zoezi la ushirikishaji jamii/wadau lilianza mwaka 2017 katika hatua za awali za mradi na kuendelea kabla na baada ya **Upembuzi Yakinifu wa Awali** (Pre-feasibility Study).

Taarifa hii inazingatia Mwongozo wa ushirikishaji Jamii wa Miradi ya Ubia (Tanzania PPP Community Engagement Framework) unaoelekeza utambuzi wa wadau, upokeaji wa maoni/michango na jinsi michango/maoni yao yalivyofanyiwa kazi katika utekelezaji wa miradi ya ubia (PPP).

MAELEZO YA MRADI

Lengo la mradi pendekezwa ni kujenga soko la kisasa lenye nafasi ya kutosha kwa wafanyabiashara wote na kutatua changamoto ya msongamano wa wafanyabiashara na wateja, Upungufu wa maegesho ya magari, Huduma zisizojitosheleza za kijamii kama Uondoshaji wa taka Ngumu, Vyoo na mifumo ya maji taka.

Soko jipya litajengwa kwenye eneo lilipo soko la sasa, ambalo linapatikana katika Kitalu Namba 1, Block AA, Mtaa wa Matumbi Kata ya Temeke. Eneo linajumla ya hekari 2.5(20,587sqm). Linamilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya

Temeke. Mradi utahusisha uhamishaji wa wafanyabiashara kwa muda wakati soko likijengwa. Eneo watakalohamishiwa linakadiriwa kuwa umbali wa mita 300 toka lilipo soko la sasa na linaukubwa wa hekari 4.

Soko jipya litakuwa na uwezo wa kuchukua aina zote za wafanyabiashara wa jumla na wa rejereje, Pia litakuwa na eneo kubwa la kuuzia vyakula, Mboga mboga na mahitaji ya nyumbani. Pia litakuwa na Vyoo, eneo la kupaki magari na eneo lakuhifadhia taka.

Mradi unatarajiwa kujengwa na kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 36 na utaendeshwa na mtu binafsi kwa njia ya ubia kati ya serikali na sekta binafsi kulingana na makubaliano ya mkataba.

Picha ya Angani kuonesha Eneo la Mradi na kuwahamishia kwa muda (Eneo la Mradi limeoneshwa kwa rangi
Eneo lililozungushiwa rangi nyekundu

HATUA YA 1: MADHUMUNI YA USHIRIKISHAJI JAMII/WADAU

Timu ya Mradi ilitekeleza ushirikishaji jamii/wadau ili kufanikisha malengo yafuatayo: -

1. Kuwafahamisha wafanyabiashara kuhusu mpango wa maboresho ya soko;
2. Kupata maoni yao kuhusiana na mradi juu ya muundo wa soko, mpangilio wa soko jipya na utayari wa kulipia ada mpya za soko baada ya soko jipya kukamilika;
3. Kupata maoni na kuwaandaa wafanyabiashara kwa ajili ya kuwahamisha kwa muda katika kipindi cha ujenzi;

HATUA YA 2: UTAMBUZI WA JAMII/WADAU

Soko la Temeke Stirio liko Mtaa wa Matumbi, Kata ya Temeke na lina wafanyabiashara zaidi ya 1,700. Timu ya Mradi wa Halmashauri iliendesha zoezi la utambuzi jamii/wadau wenye viwango tofauti tofauti vya maslahi na ushawishi katika uboreshaji wa soko la Temeke Stirio, kama inavyoonekana katika orodha ifuatayo;-

1. Wafanyabiashara waliopo sasa katika soko
2. Wateja
3. Madreva wa magari ya mizigo
4. Watumishi na viongozi wa serikali
5. Mashirika ya Kiserikali kama vile TANESCO, DAWASCO,
6. Majirani
7. Jeshi la zimamoto
8. Watu usalama mahali pa kazi (OSHA)

HATUA YA 3: UCHAMBUZI WADAU KWA KUZINGATIA KIPAUMBELE

Katika kipindi hiki cha mradi na kwa kuzingatia aina ya michango na taarifa zilizohitajika; kipaumbele kilitolewa kwa wafanyabiashara wa soko na wadau wengineo kama vile TANESCO, DAWASCO na wengine muhimu kama inavyoonekana katika jedwali Na 1.

Jedwari Na.1

AINA	**WADAU**
Nishati na Wakala	DAWASCO, Jeshi la zimamoto, OSHA
Serikali za mitaa	Manispaa ya Temeke, Kamati ya Maendeleo ya Kata na Ofisi ya mtaa.
Jamii inayozunguka mradi / Majirani	Jirani # 1 Jirani # 2

Wafanyabiashara / wachuuzi	13
Wadau wengine	Taasisi za kifedha, Msikiti, Hospitali ya Rufaa ya Temeke na vituo vingine vya afya vilivyo karibu na mradi.

HATUA YA 4: NJIA (MBINU) ZILIZOTUMIKA KUSHIRIKISHA JAMII NA WADAU

Ili kufaninikisha zoezi la ushirikishaji jamii na wadau, Timu ya Mradi ya Halmashauri (PPP Project Team) iliwashirikisha wadau kupitia mbinu mbalimbali mathalani Mikutano ya hadhara, mikutano ya makundi, mazungumzo ya ana kwa ana n.k kama inavyo onekana hapo chini: -

Mikutano ya jamii

Kuanzia 2017 mpaka sasa, Mikutano zaidi ya mitano imeshafanyika ambayo imehusisha wadau mbalimbali ndani ya soko kwa kuzingatia makundi yao ili kuwashirikisha kikamilifu juu ya mradi.

- Mikutano yote mitano ililenga kupata maoni ya wafanyabiashara waliopo, wateja na wadau wengine muhimu juu ya uboreshaji wa michoro ya awali ya soko jipya.
- Mikutano ilitumika kutoa taarifa za mradi hatua kwa hatua. Mikutano zaidi itafanyika kuwataarifu wafanyabiashara na wadau muhimu juu ya hatua za ufanyaji wa Tathimini ya Athari za kimazingira na kijamii. Maoni ya wadau yalitumika na kuingizwa katika TAMJ.
- Mrejesho utatumika katika upembuzi yakinifu kukamilisha michoro ya soko jipya.

<u>Vikao vitakavyofuatia:</u>

Timu ya Mradi itaendelea na utaratibu wa kufanya vikao vya jamii na wadau katika hatua zinazofuata ikiwa ni pamoja na kutoa mrejesho wa jinsi maoni ya awali yalivyofanyiwa kazi hasa katika ubunifu wa michoro ya mradi na jinsi gani itakavyotumika katika hatua ya upembuzi yanifu.

Mahojiano ya Mtu mmoja mmoja

Timu ya Mradi imeweza kuendesha mahojiano ya mtu mmoja mmoja katika kipindi cha miezi kumi iliyopita hususani Mwezi Mei 2019. Watu walioshiriki mahojiano haya ni pamoja na viongozi wa mitaa, Kata, maafisa wa Halmashauri, Afisa wa Wakala wa usalama mahala pa kazi (OSHA), Maafisa wa Mamlaka ya maji safi na maji taka Dar-es-salaam (DAWASA).

- Mahojiano yalilenga katika kutoa taarifa kuhusu mradi pamoja na kukusanya maoni juu ya michoro ya awali ya soko;
- Aidha, wadau hao walijulishwa kuhusiana na mchakato wa TAM ili kukusanya taarifa mbalimbali ambazo zitaingizwa kwenye andiko la taarifa ya wigo wa mradi (scoping report) na hadidu za rejea za tathimini ya athari za mazingira.

Majadiliano ya Vikundi (focus group discusion)

Kati ya Mwezi January na Mei 2019, timu iliweza pia kufanya mahojiano ya vikundi na wadau mbalimbali kupata maoni yao juu ya Michoro/Muundo wa mradi. Wadau hao ni: -

- Wafanyabiashara, Wateja, Viongozi wa serikali ya mtaa,
- Jamii inayozunguka Mradi na Wafanyabiashara walio karibu na eneo watakalohamishiwa kwa muda (Mwembe Yanga)
- Wafanyabiashara walio mkabala na Mradi

Mwaka 2020; Timu ya Mradi inaendelea kutambua na kuvishirikisha vikundi vingine katika hatua zingine zinazofuata mathalani Upembuzi Yakinifu.

HATUA YA 5: UFUATILIAJI NA USHUGHULIKIAJI WA MALAMIKO/KERO ZA WADAU

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Ushirikishaji Jamii/Wadau katika miradi ya Ubia (PPP Community Engagement Framework), ushughulikiaji wa maoni/kero za jamii na wadau unazingatia taratibu maalumu.

- Halimashauri ya Manispaa ya Temeke pamoja na kuwa na kitengo cha malalamiko itaanda utaratibu maalum wa kushughulikia malalamiko yanayo husiana na Mradi wa Uboreshaji wa Soko la Sterio.
- Mchakato utaendana na mchakato wa kushughulikia malalamiko ulioanishwa kenye miongozo ya kiusalama (RPF and ESMF) kwa ajili ya miradi ya Ushirikishwaji wa sekta binafsi ya Tanzania (TPPP);
- Kwa sasa tumeanza kuandaa utaratibu maalumu wa kushughulikia malalamiko kuhusiana na Mradi wa Temeke Sterio na baadae mafunzo maalum yatafanyika kwa watu mbalimbali watakaohusika na ushughulikiaji wa kero/malalamiko/maoni.

Kwa sasa mradi unaendelea kutumia mfumo uliopo wa kushughulika na maoni/malalamiko/kero wa Halmashauri ya Manispaa, ambao huanzia ngazi ya mitaa, kata hadi ngazi ya Halmashauri.

HATUA YA 6: TAARIFA ZA MASWALA/MICHANGO/MAONI YALIYOIBULIWA NA WADAU KATIKA HATUA ZA USHIRIKISHWAJI JAMII

Sambamba na malengo ya ushirikishaji wa jamii na wadau katika kufanikisha Maboresho ya Soko la Temeke Sterio; michango na maoni mbalimbali ya wadu yalitolewa kati ya mwaka 2017 na Disemba 2019 kama yanavyoainishwa katika jedwali Na. 2 hapo chini: -

Jedwali na 2.

UHUSIANO WA MRADI	MCHANGO/MAONI/HOJA	MAJIBU YA MAONI/HOJA/MCHANGO
Occupational Safety and Health Authority (OSHA	- Zahanati au Chumba ha Huduma ya kwanza kiingizwe katika Michoro ya ujenzi ili kutoa huduma kwa wafanyabiashara ili kuongeza uzalishaji - Kuunda kamati za usalama na afya kwaajili ya kusimamia maswala yote ya kiafya na usalama wa soko. - Soko jipya liwe na hewa ya kutosha - Kabla ya kuanza ujenzi michoro ya soko ipeleke OSHA kukaguliwa - Lifti itumike kubeba mizigo kupandisha juu ya jengo badala ya kubebwa na wafanyakazi. - Mradi usajiliwe OSHA kabla ya Mkandarasi kuanza ujenzi. - Sera ya Usalama mahali pa kazi ibandikwe ubao wa matangazo.	- Michoro wa soko utazingatia mapendekezo yalitolewa kipindi cha upembuzi yakinifu. - Mahitaji yote yanayohitajika yatatekelezwa katika vipindi vyote vya mradi ipasavyo.
Jeshi la Zima moto	*Kabla ya ujenzi ilipendekezwa:-* - Kuwe na michoro ya usanifu majengo. - Mpangilio sanifu - Kuwe na mifumo ya kuzimia moto iliyoandaliwa na mtalaam anayetambulika na itakayo hakikiwa na zima moto *Kipindi cha ujenzi;-* - Wafanyakazi kupatiwa mafunzo ya awali ya zima moto - Kufunga mifumo ya kukabiliana na moto kulingana na michoro iliyohakikiwa na jeshi la zima moto - Kutoa vifaa kinga kwa wafanyakazi,mitungi ya zima moto na vifaa vya huduma ya kwanza *Baada ya ujenzi;-* - Mafunzo ya msingi ya kukabiliana na moto yatolewe kwa wafanyabiashara wote - Kufanya ukaguzi kwa kila hatua	Mshauri elekezi atashauriwa kutimiza mahitaji yote kukidhi vigezo vya usajili.

Dar es salaam Water and Sewerage Authority (DAWASA)	- Eneo lote lijengewe mitaro ya maji ya mvua - Mifumo ya maji taka iunganishwe katika mifumo ya DAWASA badala ya kutumia mashimo ya maji taka ili kupunguza gharama za kunyonya maji taka - Badala ya kutumia kisima inatakiwa kuunganisha maji safi na salama kutoka DAWASA - Kuwe na tanki la kuhifadhi maji kwa ajili ya dharura hasa moto.	Itazingatiwa wakati wa kipindi cha upembuzi yakinifu nakuingizwa katika michoro ya mradi.
Mkuu wa Idara ya Usafishaji wa Manispaa	- Kuwajengea uwezo wafanyabiashara juu ya njia bora ya uhambuzi wa taka - Kujenga kizimba cha taka na kukigawa kulingana na aina ya taka zinazozalishwa mfano eneo la taka za plastiki, Taka zinazooza, Mabaki ya chakula na taka za vifungashio. - Kuwa na shimo kwa ajili ya kukusanyia rojo linalotokana na taka ili lisichanganyikane na majimvua na kuleta madhara kwa jamii na mazingira. - Kuishirikisha idara ya usafi na mazingira katika maandalizi ya michoro ya kizimba cha taka - Kuzingatia mapendezeshaji eneo lote la soko na kuweka maeneo ya kupumzikia wafanyabiashara/wateja - Wakati wa ujenzi vizuizi maalum vitumike kuzuia vifusi visianguke katika kipindi chote cha ujenzi.	Mshauri elekezi atashauriwa kuzingatia maoni yote yaliyotolewa na wadau na kuyafanyia kazi.
Afisa Mipango Miji wa Manispaa	- Kulingana na michoro ya mipango miji, kitalu Na 1, kimetengwa maalumu kwaajili ya soko, hivyo matumizi ya eneo kwasasa yana shabihiana na mpango wa matumizi ya ardhi husika.	Eneo ni mali ya Manispaa ya Temeke limetengwa maalumu Kwaajili ya soko.

Mtendaji wa kata	- Ameufurahia uwepo wa mradi ndani ya kata yake. - Wafanyabiashara watafutiwe eneo la kuwahamishia kabla ya ujenzi kuanza na kuhakikisha wanarudi wote pindi soko litakapokamilika kujengwa. - Kuhakikisha uwepo wa mifumo bora ya maji mvua na maji taka kuzuia milipuko ya magonjwa - Kizimba cha taka ngumu kiwe na ukubwa wakutosha kukidhi kiwango cha uzalishaji wa taka. - Kuhakikisha kuna maegesho ya magari ya kutosha na vituo vya mabasi vya kudumu viwepo katika eneo la mradi na eneo watakalo hamishiwa. - Ujenzi wa soko jipya uzingatie mahitaji ya watu malumu mfano walemavu.	Mshauri elekezi atashauriwa kuzingatia maoni yote yaliyotolewa na wadau na kuyafanyia kazi.
Mwenyekiti wa serikali ya mtaa,	- Mifereji ya maji ya ijengwe kwa ubora unaotakiwa - Kuwe na eneo la kutosha la maegesho ya magari. - Kuwe na vituo vya mabasi ili kuhamasisha wateja kufika sokoni.	Mshauri elekezi atashauriwa kuzingatia maoni yote yaliyotolewa na wadau na kuyafanyia kazi.
Watu wanaoathiriwa na mradi (PAPs)	- Kuhakikisha usalama eneo watakalo hamishiwa. - Kutoa gharama za kwa wafanyabiashara kutoka na kwenda eneo watakalohamishiwa na vile vile wakati wa kurudi ujenzi utakapokuwa umekamilika; - Kutengeneza maegesho yakutosha kwani yaliyopo sasa hayakidhi mahitaji. - Soko jipya liwe na uwezo wa kuingiza hewa ya kutosha kukabiliana na hali ya joto ya jiji la Dar es salaam. - Kuandaa sehemu nzuri ya kuwahamishia wafanyabiashara na kutoa kipaumbele cha kuwarudisha wale wote watakaopisha ujenzi wa soko jipya pale litakapokamilika. - Walitaka wahusishwe katika hatua zote za	Maoni yamepelekwa vikao vya menejimenti kwaajili ya kupatiwa ufumbuzi.

	ujenzi wa soko jipya. - Walishauri ukubwa wa vizimba uwe futi 5.	
Majirani wa Mradi	- Waliufurahia mradi kwani utaongeza thamani ya maeneo yaliyo karibu na soko. - Kuwe na uchambuzi wa taka ili kurahisisha urejeshaji wa taka(Recycling) kwaajili ya utengenezaji mbolea na vyakula vya mifugo. - Kutenga eneo kubwa la maegesho ya magari kupunguza msongamano wa marori katika barabara.	Mshauri elekezi atashauriwa kuzingatia maoni yote yaliyotolewa na wadau na kuyafanyia kazi.

MAONI YA WAFANYABIASHARA WA SOKO LA STERIO

Katika ushirikishwaji wa jamii wadau waliibua maswala mabalimbali kama ifuatavyo;-

- Ujenzi uzingatie mapendekezo ya maeneo ya kufanyia biashara,hii ni pamoja na ukubwa vizimba kuwa angalau futi 5
- Soko jipya liwe na maeneo makubwa ya maegesho tofauti na ilivyo sasa.
- Soko liwe nafasi za kutosha ili kuruhusu hewa ya kutosha, kuendana na hali ya joto ya Jiji la Dar es salaam.
- Kuandaa eneo linalifaa la kuhamia kwa muda kupisha ujenzi, lakini kuhakikisha kuwa kila mfanyabiashara anapewa kipaumbele kupata nafasi katika soko jipya.
- Kuwepo wa stendi ya mabasi katika eneo la muda ili kuwezesha soko kupata wateja.
- Kufikiria kuhusu gharama za usafiri wa kuhamia Mwembeyanga na kurudi Temeke Sterio pindi soko litakapokamilika.
- Aidha wameshauri kuwepo na ushirikishwaji kwa kila hatua katika uboreshaji wa soko.
- Kuhakikisha kunakuwepo na miundombinu ya kuzima moto kwa kuzingatia michoro ya Kihandisi iliyo thibitishwa na mamlaka husika kwenye uboreshaji wa soko
- Alishauri Wafanyabiashara waliopo kupewa kipaumbele cha kurudi katika vizimba vyao pindi soko litakapokuwa limekamilika.
- Walishauri vizimba vya kuku viwe vya ukubwa mbalimbali wa kuweza beba kuku 150 hadi 400.
- Idadi ya vyoo iongezeke kukidhi mahitaji
- Baadhi ya wafanyabiashara walihofia ongezeko la ushuru.
- Mitaro iwe na ubora unaokidhi mahitaji.
- Baadhi ya wafanyabiashara hawakuafiki soko la ghorofa na walishauri lijengwe soko kubwa la kawaida
- Soko jipya liwe na huduma za benki
- Soko jipya liwe na machinjio na yawe eneo la chini

Hitimisho:

Hadi sasa maandalizi ya uboreshaji wa Soko la Temeke Sterio unaedelea vizuri kwa kuzingatia hatua za maandalizi ya miradi ya ubia kwa mujibu wa Sheria ya Miradi ya Ubia (PPP).

Timu ya uratibu wa Mradi inazingatia sheria, taratibu, na miongozo ya ushirikishaji jamii. Hadi sasa imeweza kukusanya maoni na itaendelea kulitekeleza hili kwa ufanisi na weledi katika hatua zinazofuata.

Kwa taarifa na maoni zaidi; tafadhali wasiliana na Timu ya Mradi kupitia mawasiliano hapa chini:

MKURUGENZI,

MANISPAA YA TEMEKE,

BARABARA YA MANDELA,

S.L.P 46343,

15883- DAR ES SALAAM.

SIMU: 255 713 418 076 or **255 717 034 351**or **255 628 981 533**

BARUA PEPE: temeke@temekemc.go.tz or **johnsonmakalanga@temekemc.go.tz**